**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFSI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA**

SHULE YA SEKONDARI WASICHANA TABORA,

SANDUKU LA POSTA 152,

**TABORA.**

21/11/2025

**Mawasiliano**

**Mkuu wa shule: 0685012512/0766598393**

**M/mkuu wa shule: 0753266236**

**Mwandamizi Nidhamu: 0759813794**

**Kumb. NA. JI/TGS/177/**

**JINA LA MWANAFUNZI……………………………………….**

**MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA TABORA WILAYA YA TABORA MKOA WA TABORA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2026**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza, katika shule hii mwaka 2026. Shule ya Sekondari ya Wasichana Tabora ipo kusini mwa kituo cha mabasi na stesheni ya reli, umbali wa km.3 toka stesheni ya reli na km.4 toka kituo cha mabasi Tabora Mjini kuelekea Kipalapala. Shule Imepakana na Sekondari ya Tabora Boys.

Kutoka stesheni au Kituo cha Mabasi mjini unaweza kukodi 'taxi' kuja shuleni nauli ni sh. 5,000/-, Aidha zipo Bajaji (pikipiki za matairi matatu) nauli ni Tsh 3000/-,na pikipiki za matairi 2 nauli azidi Tsh.1,500/= Muhula wa masomo unaanza tarehe 13/01/2026 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2026 na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 18/01/2026

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1.0 SARE YA SHULE

Mwanafunzi anatakiwa kuja na sare/ mahitaji yafuatayo: -

(i) Mashati meupe mawili yenye mikono mifupi yanayoishia kwenye kiwiko cha mkono na yasiyobana mwili.(Mashati ya mikono mirefu kwa wenye mahitaji maalumu (Wenye Ualbino)

(ii) Nguo za kuvaa ndani ya shati ambazo ni Sidiria au "vest" za rangi nyeupe au nyeusi, Haturuhusu uvaaji wa nguo zenye rangi tofauti na hizi.

(iii) Sketi ya shule rangi ya Aqua-blue namba (Hex#0080FF) yenye mshono wa rinda box kubwa mbele na nyuma, na malinda mawili kushoto na mawili kulia**. Urefu wa sketi ni kufunika kifundo cha mguu kwa wote (kitambaa kizito cha suti, unashauriwa kununua kitambaa hiki hapa Tabora kuepuka kununua kitambaa kisichokuwa sahihi, epuka kushawishiwa na muuza vitambaa kuwa ndicho sahihi zingatia namba ya kitambaa hapo juu)**

(iv) Viatu vyeusi vya ngozi pair 2 vyenye kamba, visigino vifupi. Haturuhusu viatu vingine vyenye urembo.

(v) Jozi tano za soksi nyeupe zisizo na mistari ya aina yoyote ndefu (free size / stocking zinazofika magotini).

(vi) **Wanafunzi wa Kiislamu**: Nusu kanzu nyeupe mbili za kitambaa cha tetroni nzito na hijabu (Juba) nyeupe mbili, ndefu zinazofunika kifua zisizo na urembo wa aina yoyote kwa ajili ya darasani na juba nyeusi ndefu kwa ajili ya kushindia.

(vii) Kwa ajili ya michezo: Bukta ya njano, Raba nyeupe, T-Shirt ya njano yenye kola duara**( material ya manga)** isiwe na maandishi wala michoro ya rangi yoyote ile, na sketi ya njano inayofika kwenye magoti mshono wa solo kitambaa cha tetron.

(viii) Shamba dress (Gauni) mbili rangi ya bluu nyeusi(darkblue) kwa ajili ya kushindia, urefu ni kufunika kifundo cha miguu kwa dini zote, kwa wenye mahitaji maalumu (wenye ualbino) shamba dress iwe na mikono mirefu. (kitambaa kizito cha suti, Esteem no.1)

(ix) Madaftari 12 Dozen 1 (counter Book quire 4)- wote.

(x) Boksi la kalamu ya wino na boksi la penseli-wote

(xi) Mkebe wa vifaa vya Hisabati (Mathernatical set),

(xii) Vitabu vya TIE (Taasisi ya Elimu Tanzania) kwa masomo yote.

### 2.1.1 Godoro size 2.5"x6"

- Shuka 3 (mbili za pinki na foronya zake na moja nyeupe na foronya yake.
- Mto 1
- Chandarus 4"x6" rangi nyeupe duara au pembe nne.
- Blanketi 01-
- Kopo la kuogea
- Kidau cha sabuni

### 2.1.2 Mahitaji mengine ya kibinadamu:

(1) Tranka (sanduku la chuma kwa ajili ya usalama wa vitu vyake na kufuri imara kwa ajili ya kufungia tranka.

(ii) Vyombo vya chakula (kijiko, kikombe, bakuli lenye mfuniko au container na chupa ya chai)

(iii) Picha 4 passport size akiwa amevaa shati la shule (jeupe) na ziwe na kivuli (background) cha blue nyuma.

(iv) Taulo(01 ) Vitenge au Kanga doti moja ambavyo atajifunga wakati wa kwenda kuoga.

(v) Tracksuit rangi nyeusi Jozi moja yenye mistari myeupe pembeni (ambayo atavaa wakati wa kujisomea usiku).

(vi) Sweta la rangi ya Aqua-blue sawa na rangi ya sketi lililofumwa kwa uzi mzito wa kufumia.

**(Ushauri**: Unashauriwa kununua Tabora ili kuepuka kununua sweta lisilo sahihi).

(vii) T-shirt ya shule nzito rangi ya kijivu (**material manga**) yenye shingo ya duara isiyo na maandishi yoyote.

(viii) Viatu vya kimasai kwa ajili ya kushindia vyenye mikanda miwili mfano wa kanda mbili **(yebo yebo hairuhusiwi)**

(ix) Ndala aina ya umoja kwa ajili ya kuogea tu na si vinginevyo.

### 2.2.0 MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUFANYA YAFUATAYO:

i. Mwanafunzi kuvaa vazi la Nyumbani wakati wote awapo shuleni, hivyo asije na nguo za nyumbani.
ii. Mwanafunzi kuja na **SIMU** shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi. Kwa mawasiliano Mwanafunzi awapo safarini, tumia simu ya dereva au kondakta au mtu yeyote unayemuamini aliye safarini na mwanao. Kwa mawasiliano zaidi piga 0753266236 (makamu mkuu wa shule Utawala) na 0688088301 (makamu mkuu wa shule Taaluma)
iii. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na begi la kuwakea nguo (sanduku).
iv. Mwanafunzi harusiwi kuja na pasi ya kanyooshea nguo shuleni,

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo řekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Tekinolojia na Ufundi, yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

(a) Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na Jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima

(c) Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo kwa mujibu wa ratiba ya shule.

(d). Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).

(e) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(f) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(g) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(h) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

(i) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na;

(j) Kutunza mali za shule na kuzilinda ni jambo la lazima

(k) Mwanafunzi analazimika kuhudhuria vipindi vyote vya dini kwa mujibu wa ratiba ya shule.

## 3.1 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

i. Mwanafunzi ataruhusiwa kuja nyumbani kwa ajili ya msiba wa mama, baba, Mlezi, kaka au dada (ndugu wa tumbo moja/baba mmoja) tu na siyo ndugu mwingine. Taarifa za misiba ziletwe moja kwa moja kwa Mkuu wa Shule siyo kwa mwanafunzi, Mwanafunzi hataruhusiwa iwapo utaratibu huu hautafuatwa.
ii. Ni marufuku kuvaa kandambili wakati wa chakula katika Bwało au mazingira yoyote ndani na nje ya shule, isipokuwa bafuni wakati wa kuoga na bwenini.

iii. Wageni wa mwanafunzi wanaotambulika shuleni ni wale walioandikishwa kwenye faili la mwanafunzi na wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi mara moja tu kwa muhula yaani (mara 2 kwa mwaka) siku moja kabla ya mahafali ya kidato cha sita muhula wa kwanza na cha Nne muhula wa pili kwa kuitwa na Uongozi wa shule. Wasifike shuleni endapo hawajaitwa na uongozi wa shule.

iv. Likizo zote mwanafunzi atakapolazimika kwenda likizo ni sharti arudi nyumbani kwa wazazi/walezi wake, haruhusiwi kwenda kwa ndugu (Ubalozini) kipindi cha likizo fupi wala ndefu.

v. Mzazi unatakiwa kuandaa pesa ya nauli ya kuja likizo fupi (kipindi cha Pasaka na Septemba) na likizo ndefu, mwezi Juni na Desemba na kuituma shuleni pindi tu itakapohitajika (utajulishwa ni lini utume nauli).

vi. Mwanafunzi harusiwi kuwa na urembo wa aina yoyote kama vile hereni, bangili, mkufu na pete za aina yoyote ile shuleni.

vii. Shuleni haturuhusu kusuka nywele wala kutunza nywele ndefu hivyo mwanafunzi anatakiwa kuja na nywele fupi za kuchana na kitana kidogo na asinyoe mtindo wa aina yoyote ile.

viii. Mwanafunzi awapo shule atatakiwa kulala kwenye Bweni na kitanda alichopangiwa pekee yake, ni marufuku mwanafunzi kulala au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa, akishindwa kuzingatia atafukuzwa shule.

**3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:**

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga.
3. Usagaji
4. Ubakaji
5. Ulevi na matumizi ya Madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, Cocaine, Mirungi. Kubeli na kadhalika.
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kuwa mjamzito kupata mimba
10. Kuolewa au kuwekwa kimada
11. Kutoa mimba.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki migomo na kuvuruga amani na usalama wa shule au watu wengine.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Kuwa na simu ya mkononi shuleni au kumiliki kifaa chochote kinachohusiana na simu
15. Kuhama bweni alipopangiwa na kulala bweni jingine bila ruhusa.
16. Kuhamisha taa ya umeme (bulb) kutoka eneo moja kwenda kupachika eneo jingine.
17. Kubadili dini awapo shuleni tofauti na aliyoandika wakati wa kuripoti shuleni.
18. Kutoroka nje ya shule na kwenda nyumba za starehe na kwenda sehemu zingine zisizo ruhusiwa.

## 4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKABIDHIWA SHULENI NA MWANAFUNZI

i. Fomu ya kupimwa afya yake (Form for Medical Examination) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.
iv. Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

### 4.1 Mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo:-

i. Sabuni Lita tano (5) (Dexi clear, Tarmol, Lit)
ii. Ndoo 2
iii. Ream paper 2
iv. Siko (Kotama)
v. Fyekeo
vi. Jembe
vii. Soft bloom
viii. Duma la lita tano (5) kwa ajili ya maji ya kunywa.
ix. Nakala ya cheti cha kuzaliwa (njoo na cheti halisi na nakala pia)

***Muhimu: Tafadhali njoo na fomu hii iliyojazwa ikiwa na karatasi zote kumi na tano (15),***

**FORM NO. 1**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRESIDENTS' OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical Officer in respect of all Form 1 and Form V entrants.

Pupil's full name..........................................................................................................................

Age/ Years.................................................sex....................................................................................

Blood found (red and White)………………..................................................................................

Stool examination:........................................................................................................................

Urinalysis:.......................................................................................................................................

Venereal Diseases test:..................................................................................................................

T.B. test:..........................................................................................................................................

Eye Test:.........................................................................................................................................

Chests:.............................................................................................................................................

Splean:.............................................................................................................................................

Abdomen:........................................................................................................................................

Urine for Pregnant..........................................................................................................................

ADDITIONALL INFORMATION (If any) e.g., Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc. infection chronic or family disease etc.

.......................................................................................................................................................
.......................................................................................................................................................

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature: ..........................................................................

Designation: ..........................................................................

Station...................................................... Date................................

Official Stamp..........................................................................

**FORM NO. 2**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA TABORA**

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. JINA LA MWANAFUNZI.......................................................................................................

2.KABILA...........................................................................................................................

3. TAREHE YA KUZALIWA..................................MWEZI.....................MWAKA.........................

4.  WILAYA YA KUZALIWA: ... …………………………  MKOA: ………...................................

5.DINI……………………….    DHEHEBU……………………………………………………

6. JINA LA MZAZI/MLEZI ......................................................................................................

(*Ikiwa mzazi amefariki andika jina la mlezi hapa*)

7. ANWANI YA MZAZI/MLEZI: ……………………………....................................................

KIJIJI/MTAA: ……………………………………………. KATA: ………………………………...

TARAFA: ……………. WILAYA/KATA)………………………MKOA……………………………..

Na. ya simu ya mzazi/mlezi....................................................

8. KAZI YA BABA/MLEZI…………………………………..

9. KAZI YA MAMA/MLEZI………………………………….

10. Afya ya mwanafunzi (kama ana ugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe: udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha Daktari).

Taja Udhaifu wowote WA mwili au afya Yake Na uambatanishe cheti cha Daktari).

11. Majina ya Ndugu wengine wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi (watatu tu). Anuani zao kamili Namba zao za passport zibandikwe kwenye maboksi mbele ya jina la ndugu.

a) Ndugu.........................................................................................

Uhusiano na Mwanafunzi.......................................................................

Namba ya simu: ……………………………………………………....

| |
|---|
| BANDIKA PICHA |

b) Ndugu..........................................................................................................

Uhusiano na Mwanafunzi...........................................................................

Namba ya simu:…………………………………………………………

BANDIKA PICHA

c) Ndugu.........................................................................................................

Uhusiano na Mwanafunzi...........................................................................

Namba ya simu:……………………………………………………………

BANDIKA PICHA

**SAINI YA MWANAFUNZI: .....................................**

**TAREHE…………………………….........**

**FORM NO. 3**

**MKATABA AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi………………………………………….. (jina kamili) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii. Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote. Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

Jina la Mwanafunzi…………………………………………………….

Saini ya mwanafunzi…………………………………………………..

Shahidi…………………………………………………………………

Jina kamili……………………………………………………………..

Saini……………………………………………………………………..

Tarehe…………………………………………………………………

**FORM NO. 4**

**A: AHADI YA MZAZI:**

Mimi.......................................................(Jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi wa……..……………..………..

Kidato cha……………… Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hil. Nashidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaads kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo. Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule

Saini ya Mzazi/Mlezi…………………………………………………

Anuani kamili…………………………………………………………

Simu ………………………………………………………………….

Tarehe…………………………………………………………………

**NB**: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. **TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI /MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWEL WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:- 0753266236 (makamu mkuu wa shule Utawala) na 0688088301 (makamu mkuu wa shule Taaluma)**

➤ Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII

MWL LYDIA ELIUD MWAMPAMBA

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA TABORA
S.L.P. 152
TABORA